UTANGULIZI ... 2
MRADI WA UFUGAJI WA KUKU ... 3
Mazao ya kuku ... 3
Aina ya miradi ya kuku ... 3
UFUGAJI WA KUKU WA ASILI ... 4
MAHITAJI MUHIMU KATIKA UFUGAJI WA KUKU WA ASILI ... 4
Nini ufanye ili ufuge kuku wa asili kwa Faida? ... 5
Vigezo vya kuchagua kuku bora hivi hapa: ... 5
Namna ya kuboresha kuku wa asili ... 5
Mfano wa banda la kuku lenye mwanga wa kutosha ... 6
Viota vya kawaida kwa kuku kutagia mayai ... 6
UTUNZAJI WA VIFARANGA KWA KUKU WA ASILI ... 7
UFUGAJI WA KUKU WA KISASA ... 7
Kuku wa nyama ... 8
Kuku wa mayai ... 8
ZINGATIA HAYA KWA KUKU WA NYAMA(BROILER) ... 10
UFUGAJI WA KUKU WA MAYAI ... 10
MAZOEA YANAYOWAGHARIMU WAFUGAJI ... 12
MBINU ZA KUKINGA KUKU DHIDI YA MAGONJWA ... 13
KANUNI ZA KUONGEZA FAIDA KATIKA UFUGAJI KUKU ... 14
Ugonjwa wa Newcastle(kideli) ... 15
Minyoo ... 15
Wadudu kama viroboto,Utitiri na chawa ... 15
Magonjwa ya mapafu ... 16
Ndui ya kuku/ fowl pox ... 16
Ukosefu wa vitamin A ... 16
Mafua ya kuku/infectious coryza ... 16
Homa ya matumbo/fowl typhoid ... 17
HIZI NDIZO DAWA ZA ASILI KWA KUKU ... 17
Baadhi ya Mimea inayotibu Maradhi ya Kuku: ... 18
MFANO WA KUTENGENEZA CHAKULA CHA KUKU KWA MFUGAJI ... 22
PLAN ZA MABANDA YA KUKU ... 22

## UTANGULIZI

Kuku ni mifugo kama mifugo mingine, ufugaji wa kuku umezoeleka duniani na watu ufuga kwa malengo tofauti na mitaji tofauti.
Kuna wanaofuga kwa ajili ya mboga na hawa wanafuga kuku wachache tu, kuna wanaofuga kwa kujaribisha kama mradi wa biashara, kuna wanaofuga na kufuatilia mradi kwa makini sana na kutumia mbinu za kisasa za ufugaji bora.

Kuna ufugaji wa kuku wa kawaida kama tunavyowaita wa kienyeji, hawa kuku mara nyingi hujitegemea kupata chakula na wengine upewa chakula na wamiliki, kuku hawa ufuga kiasi si wengi.

Kuna pia ufugaji wa kuku wa kisasa au lugha ya kizamani kuku wa kizungu, ila waite wa kisasa kwani kuku ni kuku tofauti ni uzalishaji wa kuku.

Ufugaji wa kuku ni shughuli inayowapatia fedha za kujikimu na kuendesha maisha watu wengi duniani kwani ni mboga inayotumiwa na watu karibu wote duniani.

Kitabu hiki kitaelekeza kwa muhtasari mbinu muhimu za ufugaji wa kuku kwa faida ikizingatiwa kufuga kwa kanuni za kisasa na maradhi ya kuku bila kusahau tiba za maradhi hayo ili mfugaji haweze kupata faida inayoendana na juhudi zake bila kusahau mtaji aliyotumia katika mradi wa kuku.

Soma kitabu hiki kwa makini kwani umefanyika utafiti wa kutosha kuhusu ufugaji wa kuku wenye tija kwa mfugaji.



# MRADI WA UFUGAJI WA KUKU

Nyama ya kuku na mayai vina soko kubwa nchini Tanzania na nchi jirani, tunaona kila sehemu chips mayai na kuku, je kuku hawa wanatoka wapi?
Kuku na mayai vinatakiwa kila kukicha kwani bila kuku na mayai hakuna mboga ya kuku wala chips mayai.

Miji mikubwa na midogo nchini Tanzania kila siku mayai na kuku vinatakiwa kwenye vibanda vya chips, migahawa na mahotelini, kwa hali hiyo ufugaji wa kuku uzalisha mauzo makubwa kwa aliyejipanga kufuga kwa faida.

Kutokana na wingi wa watu nchini Tanzania kuku wanaofugwa hawatoshelezi uhitaji wa kuku na mayai nchini Tanzania, kwa hiyo juhudi za makusudi zinatakiwa kuwapa elimu wafugaji na wanaotaka kufuga ili wazalishe zaidi kukidhi soko lililopo kwa sasa kwa ufugaji wa kisasa zaidi na kanuni kuzingatiwa ili kupata faida zaidi.

## Mazao ya kuku

Mazao yatokanayo na kuku ni haya yafuatayo:

- Mayai
- Nyama ya kuku
- Manyoya
- Mbolea

## Aina ya miradi ya kuku

Kuku wanaweza kugawanwya katika aina mbili

- Kuku wa asili, maarufu kama kuku wa kienyeji
- Kuwa wa kisasa, maarufu kama kuku wa kizungu

Aina ya Kuku wa asili



Aina ya  Kuku wa kisasa



Kuku wa asili wako wa aina tofauti na kuku wa kisasa wanakuwa bora na kuwa na uzito kwenye mzani pia kuweza kutaga mayai kila siku kama ni kuku wa mayai ikiwa huduma inayotolewa kwa kuku inafuata kanuni ya virutubisho vya aina zote muhimu kwa chakula cha kuku.

Kuku wa kisasa wapo wa mayai na nyama, kwa hiyo kama ni kuku wanyama inapashwa wapewe chakula cha kuwakuza haraka na kuwapa virutubisho stahiki kikanuni za lishe wa kuku wa nyama, kuku wa kisasa wa mayai hivyo hivyo wanastahili wapewe virutubisho stahiki.

## UFUGAJI WA KUKU WA ASILI

Kuku wa asili wanaweza wa kufugwa kwa njia tofauti na malengo tofauti, kama ni kwa ajili ya mboga na mayai ya familia basi itakuwa ufugaji wa kuku wa chache, kama ni kwa ajili ya biashara basi ufugaji ni wa kuku wa asili wengi na huduma ya uhakika kama mradi.

Ufugaji wa kuku wa asili waweza kuwa huru kwa kuku kutafuta chakula wenyewe au kuwatafutia na kuwawekea kwenye banda maalum.

Kuku wanakuwa huru kujitafutia chakula popote ili mradi sehemu iwe salama na isiwe yenye mazao wanayokula kuku, pasiwe na wanyama wala kuku na wezi.



Kuku wa asili wakijitafutia chakula wenyewe



Ufugaji wa Kuku wa asili kwa kupewa chakula

## MAHITAJI MUHIMU KATIKA UFUGAJI WA KUKU WA ASILI

- Maandalizi ya kufugia
- Chakula cha kuku
- Chanjo
- Tiba wakipata magonjwa

## Nini ufanye ili ufuge kuku wa asili kwa Faida?

- Kwanza andaa banda bora la kufugia
- Chagua kuku wa asili walio bora na wasio na magonjwa
- Watunze na walishe chakula chenye kuzingatia virutubisho muhimu
- Hakikisha unawachanja na kudhibiti dalili za magonjwa

## Vigezo vya kuchagua kuku bora hivi hapa:

- Kuku wanaohimili magonjwa
- Kuku wenye kukua haraka wakila chakula sahihi na kunenepa haraka ili wawe na uzito
- Kuku wenye uwezo wa kutaga mayai angalau yai moja kila siku
- Kuku wenye kuhatamia mayai na kulea vifaranga pindi ukiamua kuongeza uzalishaji wa kuku

## Namna ya kuboresha kuku wa asili

Kuku wa asili wanaweza kuboreshwa kwa kutumia jogoo wa kisasa ,hawa kuku watakao zalishwa wanawaita chotara kwa lugha rahisi.

Ukiamua kuendeleza kuku wa asili pekee basi utachunguza kuku waliozalishwa na kuku mwenye sifa za kutaga mayai mengi na kuyahatamia yakatoa vifaranga.
Kwa hiyo ukianza kufuga kuku wa asili hakikisha kuwafuatilia kuku wako kujua sifa kiuzalishaji na kiuleaji wa vifaranga ili ukianza kuchagua mbegu bora kuiendeleza uwe una picha halisi.

Hakikisha majogoo yanakuwa ya aina tofauti kwenye banda la kuku ili upate uwezo wa kutambua sifa za jogoo wenye uwezo wa kuzalisha kuku bora kwa matetea, kwa hiyo ufugaji wenye faida wa kuku wa asili si kuachia watoto au wafanyakazi pekee, bali na wewe uwe na rekodi ya kila mara pindi unapoanza mradi huu, mradi huu ni kama miradi mingine yenye kuleta faida na kuleta utajiri ikiwa utaujali na kuwa makini.

Ukiwa unaanza mradi wa kuku wa asili utakuwa na shughuli ya ufuatiliaji ila baada ya muda utazoea na kujua kanuni muhimu kisha kutambua kuku bora wa asili kuendelea nao kiasi kwamba itakuwa kazi nyepesi baada ya ufugaji wa hatua ya kwanza na kuendelea kwa mradi wako wa kuku wa kisasa.

**Tahadhari:** Chunga kununua kuku wapya na kuwachanganya na kuku waliopo, utaleta magonjwa kwa kuku ulioanza nao, muhimu wachanje na watenge kwanza ili kulinda magonjwa ya kuambukiza.
Banda la kuku wa asili laweza kuwa la kujenga au chumba chenye mwanga wa kutosha kama utahamua kuwafuga kama mradi rasmi wa kupata faida endelevu.

## Mfano wa banda la kuku lenye mwanga wa kutosha



banda la kuku liwe na sehemu za kutagia na kuatamia mayai, hii itasaidia usalama wa mayai na kujua kuku wapi wametaga mayai yapi kwa kuhakikisha sehemu ya kufugia ina vyumba vidogo yaani chemba maalum kama unavyoona hapo kwenye banda hilo hapo juu.
Vyombo vya kulishia chakula na vyombo vya maji ni muhimu bandani na hakikisha viko safi.

Uzalishaji wa kuku zaidi utegemea mayai ya kuku na kwa kutumia kuku wenyewe kuatamia mayai kwa siku 21 kisha utotoa vifaranga kwa ajili ya kuvikuza na kuwa kuku wakubwa kwa ajili ya nyama au kuzalisha mayai zaidi
Tunaweza kutotoa vifaranga kwa mashine ziitwazo incubator, kama Flat Table incubator, Cabinet incubator, n.k.

Sehemu ya kuweka incubator iwe imara yenye sakafu imara na kuta zisizopitisha hewa na vumbi kiasi kwamba matofali yawe yamezibwa na madirisha imara.

Kama kuku ataatamia mayai kwa ajili ya kuzalisha vifaranga basi hakikisha chakula na maji yanakuwepo karibu muda wote ili kuku asiache mayai kwa muda mrefu bila kuyaatamia ya kaharibika, pia chagua mayai yenye sifa zifuatazo:

- Yawe na ukubwa wa kuridhisha
- Yasiwe yamepasuka/nyufa
- Yawe na ganda gumu. Siyo tepe tepe

Kuku akianza kugagania kutotoka kwenye kiota cha mayai na kuanza kukusanya mayai yake hapo alipo kwenye kiota basi utaanza kumsikia akitoa sauti ya kuatamia, basi mkague kama anao wadudu na ugonjwa wowote ili atibiwe kabla ya kuatamia mayai, kwani waweza pata hasara kubwa uko mbeleni katika uzalishaji wa vifaranga kutokana na mayai yanayoatamiwa na kuku mgonjwa.

## Viota vya kawaida kwa kuku kutagia mayai



Viota ni mahali ambapo kuku hutaga mayai, kuhatamia na kuangua vifaranga. Hii inamaanisha kuwa viota ni sehemu muhimu sana ya kuzingatia ili kuweza kupata mayai mengi yaliyo salama pamoja na vifaranga.
Kuku anapotagia porini, mayai huliwa na wanyama kama vile nyoka na wengineo.

- Kwa kuwa na viota vya kutosha itapunguza usumbufu wa kuingia kukusanya mayai kwa mfugaji.
- Njia mojawapo ya kuzuia kuku kula mayai.
- Upotevu wa kuku na mayai utapungua.
- Utapata mayai bora kwa ajili ya kutotolesha.
- Kupunguza mayai kupasuka, pia mayai kuwa safi.

Mayai yasikae kwenye viota, kila siku yakusanye na uyahifadhi sehemu salama ili baadaye uyauze au uyawekee kuku akianza kuatamia.

## UTUNZAJI WA VIFARANGA KWA KUKU WA ASILI

Vifaranga vya kuku huitaji joto, chakula, maji na uangalizi zaidi ili vikue na afya kwa kupata kuku bora na wenye kuleta tija.

Hakikisha ulinzi wa wanyama kama paka shume, vicheche na wengineo, kama vifaranga wanakaa na mama yao basi hakikisha kwa mwezi mmoja unaweka vifaranga na mama yao sehemu salama kikiwepo chakula na maji muda wote.

Vifaranga wapewe chakula stahiki kama vifaranga, baada ya miezi miwili wapewe chakula cha kawaida kama kuku wanokua.

Waweza kuulizia maduka yanayouza vyakula vya kuku ili wakupe chakula cha vifaranga kilicho tayari na vipimo sawa kwani wanajua na wana uzoefu wa kuuza vyakula hivyo, pia ulizia mwenye kufuga kuku wa asili wa muda mrefu atakuonyesha sehemu ya kununua vyakula vya kuku vinavyostahili.

Kama utaamua kukuza vifaranga vingi itabidi uandae vitalu vya kulelea vifaranga na kuhakikisha kuna mwanga wa kutosha kati kati ya kitalu yaani chumba maalum cha kulelea vifaranga vya kuku hasa chemli inafaa zaidi kwani ina mwanga na joto la kutosha, waweza tumia taa za umeme kama usipotumia chemli ila hakikisha taa ina nguvu kubwa na itoe mwanga wa kutosha ukiambatana na joto la kutosha.

## UFUGAJI WA KUKU WA KISASA

Kuku wa kisasa wako wa aina mbili:

Kuku wa nyama
Kuku wa mayai

## Kuku wa nyama

Jina maarufu uitwa Broiler na wanakua kwa haraka na ndo chanzo cha nyama ya kuku kwenye miji mingi hasa ukisikia chips kuku, kuku anatokana na hawa kuku wa nyama, kuku wanyama ukua na kuwa tayari kuuzwa kwa ajili ya nyama kwa siku 50 hadi 56 ikiwa watalishwa vyema na hii inategemea vifaranga vilitunzwaje na muda gani vilianza kulishwa na kwa kutumia vyakula aina gani ila unaweza kuzidisha siku 56 ukiamua wakuwe zaidi ingawa watazidi kula zaidi pia. Ukitaka kuku wanyama wawe vizuri na kukuwa haraka hakikisha vifaranga viko sawa kiafya na lisha chakula chenye virutubisho muhimu kwa makuzi ya kuku wa kisasa wa nyama.

## Kuku wa mayai

Kuku wa mayai kuanzia kifaranga hadi kuanza kutaga mayai ni siku 151 hado 166 na inategemea unavyowalisha, kuku hawa utaga mayai bila jogoo, si lazima wapandwe na jogoo. Kuku wa mayai utaga kila siku mpaka wazeeke na kuacha kutaga, hapo ndipo unawauza kwa ajili ya nyama ili wapishe wengine kuku wachanga kwa ajili ya kutaga mayai kama biashara inavyokuruhusu.

## HATUA ZA UFUGAJI WA KUKU BORA WA NYAMA (BROILER)

Mambo ya kuzingatia kabla vifaranga wako hawajafika kwenye sehemu ya ufugiaji
· Banda la kuku, mazingira yanayolizunguka na vyombo vyote yapaswa kusafishwa vyema kwa maji safi na dawa ili kuua vimelea ambavyo vinaweza sababisha magonjwa.
· Hakikisha sehemu ya kuwekea vifaranga inapashwa kuwekwa joto kwa saa moja kabla ya vifaranga kuingia eneo la kufugia.
· Kwa matokeo mazuri na yenye faida vifaranga vyapaswa kufikishwa kwenye banda haraka iwezekanavyo na kama inawezekana wapewe chakula muda huo huo.
· Kamwe usisafirishe vifaranga kwa kutumia buti la gari mara nyingi vifaranga husafirishwa wakiwa wamewekwa kwenye seat ya gari ambapo watapata hewa ya kutosha.
· Nafasi ya vifaranga inatakiwa kuwa vifaranga kumi kwa mita square moja, epuka kuwajaza kuku wengi katika eneo dogo.

## Mambo ya kuzingatia baada ya vifaranga kufika eneo la kufugia

· Mara wafikapo tu vifaranga wanatakiwa kuondolewa kwenye box mara moja.
. Kwa siku saba za mwanzo wape mwanga kwa masaa23 ili kuwawezesha vifaranga kuzoea mazingira na kuwafanya waanze kula chakula.
· Wape maji na chakula baada ya vifaranga kuingia bandani na hakikisha unaongeza vitamin kwenye maji au glucose kabla ya kuwapa hao vifaranga.
· Hakikisha unapanga vyema vyombo vya kuweka chakula na vyombo vya maji katika mpangalio ambao utawawezesha vifaranga kula na kunywa maji vizuri.

### JOTO

· Nunua kipima joto yaani thermometer na kiweke katika urefu unaozidi vifaranga kidogo lakini iwe mbali na heater or chanzo chochote cha joto.
· Rekodi joto la kila siku kwa kawaida joto sahihi la vifaranga linapaswa kuwa kati

ya 40-41 degree centrigrade. (na njia sahihi ya kupima joto la vifaranga chukua miguu ya vifaranga na uweke katika shavu au shingo lako ukisikia miguu ina joto jua vifaranga wapo kwa joto sahihi lakni ukisikia miguu ni ya baridi basi jua ya kwamba vifaranga wanahitaji joto zaidi na hivyo unashauliwa kuongeza joto).

· Joto ni muhimu sana katika ukuaji wa vifaranga kwa wiki ya kwanza na hivyo ni vyema kulifuatilia kila siku kuepuka vifo visivyotarajiwa.

## RATIBA-MWANGA

UMRI(SIKU) ....................... MASAA

0-7 ---------------------------------------------------->0

8-21--------------------------------------------------->9

22 ------------------------------------------------------>8

23 ------------------------------------------------------>7

24 ------------------------------------------------------>6

5 SIKU KABLA YA KUUZA ------------>5

4 SIKU KABLA YA KUUZA -----------> 4

3 SIKU KABLA YA KUUZA ------------>3

2 SIKU KABLA YA KUUZA ------------>2

1 SIKU KABLA YA KUUZA ------------>1

Unashauriwa kuwapima uzito vifaranga/kuku wako kila wafikishapo siku ya 7,14,21,28 na 35

### MAJI

Maji ni muhimu kwa kuku, kuku kutokunywa maji ni kielezo tosha ya kwamba kuku wako wana shida na tafuta sababu haraka ya kutokunywa maji.

· Kwa kawaida inatakiwa vifaa 4 (drinkers) kwa kuku 100 na hakikisha maji ni masafi na salama na yanapatikana katika banda kwa masaa yote na upungufu wa maji hupelekea kuku kudumaa.

### CHAKULA

· Chakula kinapaswa kuwekwa katika magazeti au magunia safi na salama kwa siku saba za mwanzo kuwawezesha vifaranga kula chakula na baada ya siku saba anza kuwawekea chakula kwenye sehemu za kulishia(Feeders). Kwa kawaida inashauriwa kuweka tray 4 za chakula kwa vifaranga mia moja.

· Kwa feeder za kawaida inashauriwa kuwa feeders 3 kwa kuku 100, na hakikisha chakula kinahifadhiwa sehemu salama mbali na mwanga, majimaji na panya. Epuka kuwalisha vifaranga chakula ambacho kina unyevu unyevu au fangasi.

· Ili kufahamu kama vifaranga wako wanakula, chukua vifaranga 5 kama sampuli waangalie baada ya masaa 8 , tena masaa 24 kama wamekula na hii hufanya kwa kugusa mfuko wa chakula taratibu ukikuta mfuko wa chakula uko umetuna na unagusika jua ya kwamba wamekula na kinyume ya hapo ni hawali.

## AINA YA CHAKULA KWA VIFARANGA

· **Chick starter**

Wape 0.5kg kwa kifaranga kimoja kwa muda wa wiki 2

· **Grower**

Wape 1.5kg chakula cha ukuaji kwa vifaranga kwa muda wa wiki 2

· **Finisher**
Wape 1.5kg chakula cha umaliziaji kwa muda wa wiki mbili kabla ya kuwachinja au kuwauza.

## ZINGATIA HAYA KWA KUKU WA NYAMA(BROILER)

### SIKU 1-5
Wape glucose na mchanganyo mmoja wapo kati ya hii ifuatayo;
· Neoxyvital au trimazin
· Fluban na vitamin kama vile broiler boost au aminovit au supervit broiler au vitalyte

### CHAKULA
· Weka vigostart ambayo ina ridocox kwenye chakula, kilo moja kwa mfuko kuanzia wiki ya kwanza hadi nne ili kuzuia coccidiosis, baada ya kuacha endelea kutumia ridocox 200g/tani kwa kuzuia coccidiosis hadi wiki 1 kabla kuwauza kwa nyama.

### SIKU YA 6
· Vitamini (vitastress)

### SIKU YA 7
· Chanjo ya newcastle masaa mawili tu, halafu endelea na maji ya vitamin (vitastress)

### WIKI YA PILI
· Chanjo ya gumboro masaa wawili tu, halafu endelea na vitamin (vitastress)

### WIKI YA TATU
· Wape doxycol au ctc 20% au anflox gpld au fluban na amprolium,vitalyte au vitastress,molasses kwa siku 5-7

### WIKI YA NNE
· Hakikisha kuku wa nyama wanakuwa katika dozi kubwa ya vitamin (vitastress/vitalyte/broiler boost/supervit broiler)

### WIKI YA TANO
· Hakikisha kuku wa nyama wanakuwa katika dozi ndogo ya vitamin (vitastress/vitalyte/broiler boost/supervit broiler)

### WIKI YA SITA
· Wape kuku maji ya vitamin asubuhi na matupu jioni
· Na baada ya hapo kuku wako watakuwa wako tayari kuingia sokoni kwa ajili ya mauzo

## UFUGAJI WA KUKU WA MAYAI

Ufugaji wa kuku wa mayai unaruhusu mfugaji kununua vifaranga safi au kutumia mashine(incubator) kuzalisha vifaranga yeye mwenyewe, ila mara nyingi wafugaji wengi wananunua vifaranga kutoka kwa wazalishaji wa vifaranga.



Kuku wa mayai ili watage vizuri wanatakiwa walishwe chakula bora kwa utaratibu unaotakiwa, ukiwazidishia au kuwaongezea hawatotaga vizuri. Wanatakiwa walishwe kati na kati kulingana na umri kama ifuatavyo:-

## UMRI WA WIKI 1 -2

Katika umri huu wanapewa chakula aina ya "**Super Starter**" kwa ajili ya kuwatengenezea kinga mbadala ili waweze kuhimili mikiki mikiki ya vijidudu vya magonjwa kadri wanavyoendelea kukua, wanapewa chakula hicho kwa kiwango maalum kama ifuatavyo:-
Wiki ya 1: Gramu 12 kwa kuku mmoja kwa siku moja
Wiki ya 2: Gramu 22 kwa kuku mmoja kwa siku moja

## UMRI WA WIKI 3 - 8

Hapa wanakuwa bado ni vifaranga na wanapewa chakula aina ya "**Chick Starter**" kwa ajili ya kuendelea kuwajenga miili yao waweze kupoekea virutubisho vizuri, hii inatokana na kwamba kuna baadhi ya viini lishe vinafanya kazi ya kumeng'enya chakula na kupatikana viini lishe vingine, kwahiyo vikikosekana katika mwili wa kuku basi hata wale chakula gani bora, hawawezi kutoa mazao bora, lakini kwa kuwapa "Chick Starter" itawapelekea kuwa na virutubisho hivyo muhimu. Kiwango na ulishaji wake ni kama ifuatavyo:-
Wiki ya 3: Gram 27 kwa kuku mmoja kwa siku moja
Wiki ya 4: Gram 32 kwa kuku mmoja kwa siku moja
Wiki ya 5: Gram 38 kwa kuku mmoja kwa siku moja
Wiki ya 6: Gram 42 kwa kuku mmoja kwa siku moja
Wiki ya 7: Gram 46 kwa kuku mmoja kwa siku moja
Wiki ya 8: Gram 50 kwa kuku mmoja kwa siku moja

## UMRI WA WIKI 9 - 18

Katika umri huu kuku wanapewa chakula aina ya "**Grower Mash**" kwa ajili ya kuwakuza na kuwajenga mfumo wa uzazi kwa maandalizi ya utagaji. Kiwango cha chakula kinategemea na wiki kama ifuatavyo:-
Wiki ya 9: Gram 56 kwa kuku mmoja kwa siku moja
Wiki ya 10: Gram 62 kwa kuku mmoja kwa siku moja
Wiki ya 11: Gram 64 kwa kuku mmoja kwa siku moja
Wiki ya 12: Gram 66 kwa kuku mmoja kwa siku moja
Wiki ya 13: Gram 68 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Wiki ya 14: Gram 74 kwa kuku mmoja kwa siku moja
Wiki ya 15: Gram 74 kwa kuku mmoja kwa siku moja
Wiki ya 16: Gram 80 kwa kuku mmoja kwa siku moja
Wiki ya 17: Gram 82 kwa kuku mmoja kwa siku moja
Wiki ya 18: Gram 88 kwa kuku mmoja kwa siku moja

## UMRI WA WIKI 19 - 40
Huu ni umri ambao kuku wanataga kwa kiwango kikubwa sana (85% hadi 100%) hali ambayo inawafanya kutumia nguvu nyingi mno, hivyo hupewa chakula aina ya "**Layers Phase 1**" kwa ajili ya kufidia nguvu ya ziada wanayotumia ili waendelee kutaga kwa kiwango hichohicho. Ulishaji wake ni kama ifuatavyo:-
Wiki ya 19: Gram 92 kwa kuku mmoja kwa siku moja
Wiki ya 20: Gram 102 kwa kuku mmoja kwa siku moja
Wiki ya 21: Gram 108 kwa kuku mmoja kwa siku moja
Wiki ya 22: Gram 114 kwa kuku mmoja kwa siku moja
Wiki ya 23: Gram 116 kwa kuku mmoja kwa siku moja
Wiki ya 24: Gram 120 kwa kuku mmoja kwa siku moja
Wiki ya 25 - 40: Gram 130 kwa kuku mmoja kwa siku moja

## UMRI WA WIKI 41 - 80
Katika umri huu kuku wanakuwa wameanza kuchoka na huanza kutaga kwa kiwango cha kawaida (65% hadi 75%) hivyo hupewa chakula aina ya "**Layers Phase 2**" kwa ajili kuendeleza kiwango chao hicho kwa muda mrefu. Kiwango chao ni "Gram 130 kwa kuku mmoja kwa siku moja".

NB: Kuanzia wiki 81 na kuendelea unaweza kuwauza na kuweka kuku wengine.



## MAZOEA YANAYOWAGHARIMU WAFUGAJI

Kuna baadhi ya wafugaji huwa wanafuga kwa kutegemea uzoefu walionao katika ufugaji bila ya kujali kuwa kuna mabadiliko kila siku katika sekta ya mifugo, wengi wao huwa wanatatua kesi mbalimbali zinazotokea katika ufugaji kwa kutumia uzoefu hali ambayo inawasababishia kupata hasara kubwa isiyo ya lazima.

### Yafuatayo ni baadhi ya mazoea yanayowagharimu wafugaji:-

## 1. KUINGIZA VIFARANGA BILA MAANDALIZI SAHIHI
Wengi wa wafugaji huwa wanaingiza vifaranga pasipo kufuata utaratibu wa kitaalam katika kuandaa banda pamoja na maandalizi ya kupokea vifaranga. Na kama atabahatika kufanya usafi basi atafanya juujuu tu hali ambayo inasababisha

banda kuhifadhi vimelea vingi vya magonjwa na kupelekea kuku kuugua na kufa kuanzia wanaingia hadi kufikia kuuzwa, na hatimaye mfugaji hupata hasara kwani hutumia pesa nyingi kwenye madawa kwa kutibu na pesa nyingi kwenye chakula kwa kuchelewa kukua kutokana na kuumwa.

## 2. KULISHA BILA KUFUATA MAELEKEZO SAHIHI

Kila aina ya kuku wanautaratibu wa ulishwaji chakula, utaratibu ambao ukikiukwa huwezi kupata matokeo mazuri ya mifugo yako, ila wafugaji wengi huwa wanalisha kwa utaratibu usio sahihi ambao wao wanadhani kwamba ndio wataongeza uzalishaji wa mayai au watakuwa haraka kwa upande wa kuku wa nyama, na kuna wengine wanadiriki kutumia chakula aina moja mwanzo mwisho, yaan anaweza kutumia chakula cha vifaranga wa nyama (SUPER STARTER) kuanzia mwanzo hadi anauza kuku bila kufaham kwamba kila aina ya chakula ina kazi yake katika kila hatua ya umri. Lakini pia bila kujali kwamba analisha kwa gharama kubwa hali ambayo itampunguzia faida.

## 3. KUTIBU KWA DAWA AMBAYO SI CHAGUO KWA UGONJWA HUSIKA

Kama inavyofahamika kuwa wafugaji wa kuku wengi wamebarikiwa kwa kufaham majina mengi ya dawa za kuku, na kwa kutumia uzoefu walionao huwa wanatibu kuku wao magonjwa mbalimbali bila kupata maelekezo kutoka kwa Dokta au Mtaalam wa mifugo. Kwa kufanya hivyo hutumia dawa nyingi tofautitofauti kwa kutibu ugonjwa mmoja bila mafanikio na kupelekea ugonjwa kuwa sugu na idadi ya vifo kuongezeka siku hadi siku.

**USHAURI:** Sio kila mfugaji mzoefu anaweza kuwa Daktari, ila kila Daktari anaweza kuwa mzoefu.

## MBINU ZA KUKINGA KUKU DHIDI YA MAGONJWA

Tunafahamu kwamba magonjwa ndio chanzo kikubwa cha kukatisha ndoto za mfugaji kutokana na ughali wa bei za dawa au vifo vinavyosababishwa na magonjwa hayo. Lakini upo uwezekano wa kuyaepuka hayo ikiwa tutazingatia yafuatayo kwa uangalifu mkubwa:-

- Chanja kuku dhidi ya magonjwa mbalimbali yasiyotibika kama vile mdondo, gumboro na ndui.
- Usifuge kuku na ndege wengine kama vile bata, kanga au kwale katika banda moja. Pia usichannganye kuku wa asili na wa kisasa katika banda moja, yaan kwa mfano usichanganye kuku wa nyama(broilers) na kuku wa asili.
- Usirudishe nyumbani kuku waliopelekwa sokoni wakakosa soko kwani wanaweza kuleta magonjwa.
- Ondoa kuku wote wenye dalili za ugonjwa na uwatibu kwa dawa husika, na waliokufa wazike au wachome moto.
- Watenge kuku wageni kwa takribani wiki mbili kabla ya kuwachanganya na wa zamani.
- Usafi wa banda, vyombo vya maji na kulishia, na muhudumu ni vya kuzingatia pia.
- Zuia watu wasiohusika, au ndege kuingia au kukaribia banda.
- Kuwepo mavazi na viatu maalum vya kuingilia bandani.

- Mlangoni kuwekwe dawa ya kuulia vijidudu kwa ajili ya kukanyaga kabla ya kuingia bandani.
- Banda lipumzishwe wiki mbili kabla ya kuingiza kuku wapya.
- Wape kuku chakula bora na maji safi na salaama. Maji safi na salaama ni yale ambayo hata wewe mfugaji unaweza kuyanywa.

## KANUNI ZA KUONGEZA FAIDA KATIKA UFUGAJI KUKU

Ufugaji kuku ni biashara kama biashara nyingine, kuna wafugaji wengi wanaingia gharama zisizo za lazima katika kufuga kuku hali ambayo inawapelekea kupunguza faida yao na mara nyingine hata kutopata faida kabisa, hali hii inawakwaza wafugaji na wengine hukata tamaa kabisa ya kufuga. Lakini hayo yanasababishwa na wao wenyewe wafugaji bila wenyewe kujijua.
Kupitia somo hili tutakumbushana ni namna gani mfugaji anaweza kuzikwepa gharama zisizo za lazima katika ufugaji ili aweze kupata faida mara dufu. Zifuatazo ni kanuni za kuongeza faida katika ufugaji kuku:-

## 1. KUPATA VIFARANGA BORA

Vifaranga bora ni wale waliototolewa katiaka wakati uliopendekezwa kitaalaam hali ambayo inamjenga kifaranga kuwa na kinga asilia ya mwili ya kutosha, kwahiyo mfugaji anaweza kufuga hadi kufikia kuuza bila kutumia dawa za kutibu ugonjwa wowote zaidi ya chanjo na dawa za kuanzishia tu, hivyo ataokoa pesa nyingi za kumuita daktari na kununua madawa na faida itaongezeka siku hadi siku.

## 2. ULEAJI MZURI

Hapa tunakusudia usafi wa banda, vyombo vya chakula na maji, maji ya kunywa na muhudumu mwenyewe. Kwan magonjwa mengi ya kuku yanasababishwa na uchafu, hivyo uleaji ukiwa mzuri magonjwa hayatakuwepo na gharama za matibabu hazitakuwepo pia.

## 3. CHAKULA BORA

Mfugaji anatakiwa ahakikishe anapata chakula bora kwa ajili ya kuku wake, chakula bora ni ambacho kimekingwa na magonjwa yote na kinakuza kuku kwa wakati, lakini pia chakula bora ni kile ambaho hakisababishi mazingira hatarishi katika banda kama vile kulowesha banda. Chakula ambacho kinalowesha banda kina hatari ya kusababisha magonjwa mbalimbali kama vile coccidiosis na typhoid, hali ambayo mfugaji ataingia gharama za kutibu mara kwa mara.

## 4. KUPATA SOKO LA UHAKIKA

Ili upate soko la uhakika ni lazima uwe na tabia ya kutafuta taarifa, kwa kutafuta taarifa itakuwezesha kujua hali ya soko iliyopo ili nawe uweze kujipanga. Na kama ukiwa unategemea tu mtu aje kwako kununua mara nyingi utakuwa unalalamikia soko, na kuuza kuku wako kwa bei ya hasara. Ila kama unajua hali halisi ya soko basi hata akija mnunuzi nyumbani hatokudanganya na utakuwa na uhakika na bei yako.

Magonjwa ndio husababisha hasara katika mfumo wa ufugaji wa kuku. Kuku waliochanjwa dhidi ya magonjwa hudumisha afya bora. Jaribu kila mara kuzuia magonjwa, kwani kuzuia ni bora kuliko kuponya. Kinga yaweza kutolewa mara kwa mara (kila baada ya miezi mitatu) dhidi ya magonjwa yafuatayo:

## Ugonjwa wa Newcastle(kideli)

Ugonjwa huu ndio huathiri kuku na kusababisha hasara. Virusi vya ugonjwa huu huenea kwa kasi na rahisi kiasi cha kusababisha vifo kwa asilimia 100%. Dalili za kwanza ni shida ya kupumua , sauti kama ya kikohozi na kutokwa mate.

### Dalili

- Kuhalisha choo cha kijani na njano
- Kukohoa na kupumua kwa shida
- Kuficha kichwa katikati ya miguu
- Kukosa hamu ya kula na kunywa
- Kutoa kamasi na machozi
- Kupooza na kuzungusha kichwa na kutembea kinyumenyume
- Idadi kubwa ya vifo hadi 90%

### Kinga

- Chanjo (New Castle vaccine) kwa mpango wa siku 3, wiki 3, miezi 3
- Epuka kuingiza kuku wageni
- Choma au fukia mizoga ya kuku waliokufa kwa ugonjwa
- Zingatia usafi wa mazingira

## Minyoo

Minyoo kama chango (roundworms) na tegu (tapeworms) huadhiri kuku wa kienyeji. Kuku hukosa hamu ya chakula, mayai hupungua na magonjwa mengine hushambulia. Ni bora basi kutibu minyoo.

Mchanganyiko wa madawa ya aina tatu ndio hutumiwa kuangamiza minyoo, madawa haya nipiperazine, phenothiazine na butynorate. Madawa haya hupatikana kama vidonge (tumia kidonge 1kwa kuku mzima na 1/2 kwa vifaranga). Iwapo hautapata dawa hii, waweza kutumia Panacur audawa nyingine ya kuangamiza minyoo. Wapatie kuku dawa ya minyoo kila baada ya miezi mitatu

## Wadudu kama viroboto,Utitiri na chawa

Wadudu kama chawa au utitiri husumbua kuku katika ufugaji wa kienyeji. Chawa au utitiri husababisha harara ya ngozi, kuku walio athiriwa hupata shida na kukosa usingizi. Hali hii hupunguza kiwango cha mayai na uzito wa kuku.

Tumia asilimia 5% ya unga wa malathion kwa kupulizia kuku (puliza kwa chupa uliyo toboa matundu) pulizia kila kuku ili kuzuia chawa na utitiri (kilo moja ya unga huu yaweza kutibu kuku150). Pulizia dawa hii baada ya kila miezi mitatu, waweza kupuliza kwa wakati mmoja wa kutoa chanjo na dawa zilizotajwa hapo juu. Puliza unga huu pia kwenye viota vya kuangulia mayai.

Waweza kutayarisha 5% ya malathion kwa kuchanganya 25% ya unga wa malathion (kiwango cha kilimo) na sehemu nne za jivu kutoka jikoni.

- Nyunyiza majivu au chokaa mara moja kwa wiki mara baada ya kufagia
- Choma masalia ya mayai yaliyoanguliwa
- Nyunyiza dawa kwenye viota

• Weka maranda, majani makavu, makapi ya mpunga ya kutosha sakafuni ndani ya banda la kuku
• Fuata kanuni za chanjo
• Tenga kuku wagonjwa wakae mbali na kuku wazima

## Magonjwa ya mapafu

Magonjwa ya mapafu huathiri njia inayopitisha hewa na kuambatana mate na sauti kama ya kikohozi. Ugonjwa huu huenea pole pole. Uambukizanaji wake pia hutokea polepole na vifo sio kwa wingi. Hata hivyo, Tatizo hili laweza kusambaa hata kutoka mahali vifaranga walipoanguliwa hadi pale walipouzwa.

Tylosin19 ndio dawa inayoweza kutibu magonjwa ya mapafu. Kiasi cha milligram 35 ya tylosin hutosha kuku mmoja (kiwango hiki hufaa kuku na hata vifaranga) dawa hii hukomesha madhara yanayotokanana magonjwa ya mapafu. Tibu kuku kila baada ya miezi mitatu, waweza kutekeleza kwa wakatimmoja wa kutoa kinga na kuangamiza minyoo. Tylosin hupatikana kwa pakiti ndogo ya gramu 4.

Waweza kutayarisha dawa hii kwa kutumia maji na 35gm ya tylosin (gramu nne kwa vikombe viwili vya maji), kiasi hiki chaweza kutolewa kwa vitone kwa kila kuku.

## Ndui ya kuku/ fowl pox

Ndui huathiri sana vifaranga wanaokua hasa wakati wa mvua, Virus huambukizwa kupitia jeraha au mbu. Ugonjwa huu husababishwa na virusi na hauna tiba.

### Dalili

• Vidonda vyenye utando wa kahawia/purple kwenye sehemu zinazoonekana kama kishungi,usoni na chini ya mdomo
• Kukosa hamu ya kula
• Vifo vingi

### Kinga

• Chanja vifaranga wanapofikia mwezi 1-2 kwa kutumia chanjo ya Fowl pox vaccine
• Epuka kuingiza kuku wageni
• Zingatia usafi wa mazingira.

## Ukosefu wa vitamin A

Huathiri zaidi kuku wadogo wanaokua, macho huvimba na kutoa uchafu mzito kama sabuni ya kipande iliyolowa maji, kuku wenye ukosefu wa vitamin A hawaponi na hatimaye hufa.Mara kwa mara ugonjwa hujitokeza wakati wa kiangazi,kinga ni kuwapa kuku mchicha au majani mabichi mara kwa mara pia wape kuku wote dawa ya vitamin za kuku zinazouzwa maduka ya mifugo ili kuzuia kujitokeza kwa ugonjwa huu.

## Mafua ya kuku/infectious coryza

Hutokana na bakteria na hushambulia hasa kuku wakubwa

### Dalili
• Kuvimba uso
• Kamasi zilizochanganyikana na usaha unaonuka
• Macho huvimba na kutoa machozi na pengine upofu
• Hukosa hamu ya kula
• Mbawa huchafuka na kutoa harufu mbaya

### Tiba
Dawa za Antibiotic, sulfa na vitamin

Kuhalisha damu/coccidiosis
Husababishwa na vijidudu vya Protozoa

### Dalili
• Kuharisha damu
• Manyoya husimama
• Hulala na kukosa hamu ya kula

## Homa ya matumbo/fowl typhoid

• Kuharisha kinyesi cha kijani na nyeupe
• Kuku hukosa hamu ya kula
• Kuku hukonda
• Vifo hutokea kidogo kidogo kwa muda mrefu
• Kinyesi hushikamana na manyoya

### Tiba
Dawa aina ya antibiotic, sulfa na vitamini

### Kinga
• Usafi
• Fukia mizoga
• Usiingize kuku wageni
• Chinja kuku wote mara ugonjwa huu ukiingia na safisha banda, pia pumzika kufuga kwa miezi 6

## HIZI NDIZO DAWA ZA ASILI KWA KUKU

Madawa ya Asili yatokanayo na Mimea yanayosaidia katika Tiba na Kinga za Maradhi mbalimbali ya Kuku. Sehemu za mimea zinaweza kuwa: Majani, Magome, Mbegu, Maua au Matunda .

### Umuhimu wa kutumia tiba zenye asili ya mimea:
• Hupatikana kwa urahisi.
• Ni rahisi kutumia.
• Gharama nafuu.
• Zinatibu vizuri zikitumika vizuri
• Hazina madhara.

## Baadhi ya Mimea inayotibu Maradhi ya Kuku:

**1. Mwarobaini (Majani, Mizizi, Magome):**



Hutibu magonjwa yafuatayo:

- Typhoid.
- Kuzuia Kideri.
- Kuhara.
- Mafua.
- Vidonda.

2**. Shubiri Mwitu (Aloe vera):**



Chukua majani 3-5 makubwa, katakata na loweka ndani ya maji lita 10 kwa masaa 12 hadi 16. Wape kuku kwa siku 5 - 7.

Isiyotumika mwaga na tengeneza nyingine baada ya masaa 12.

Mchanganyiko huu unaweza kutibu:

- Kideri/Mdondo (Mdonde/Chikwemba/Kitoga/Chinoya/Sotoka) - inyweshwe kabla kwa kinga.
- Homa ya matumbo (Typhoid).
- Mafua (Coryza).
- Kipindupindu cha kuku (Fowl Cholera).

3**. Mtakalang'onyo (Euphorbia):**



Chukua Majani makubwa 3-5, ponda, weka katika lita 10 za maji kwa masaa 12-16, chuja na wape kuku. Isiyotumika mwaga na tengeneza nyingine. Mtakalang'onyo hutibu:

• Kideri/Mdondo (Mdonde/Chikwemba)
• Ndui. • Kuhara damu (Coccidiosis).

4**. Mbarika (Nyonyo):**



Hutibu Uvimbe. Weka majani ya mbarika ndani ya majani ya mgomba kisha weka ndani ya jivu la moto, kisha kanda sehemu yenye uvimbe kwa kutumia majani hayo ya mbarika.

5. **Mlonge (Mlonje):**



Ina vitamini A na C. Chukua majani ujazo wa mikono miwili (gao mbili). Kisha yapondeponde na kuyaweka katika lita 10 za maji na iache kwa masaa 12-16, chuja na wape kuku. Isiyotumika mwaga na tengeneza nyingine.

Mlonge hutibu:

• Mafua.
• Kideri - inyweshwe kabla kwa kukinga
• Kipindupindu cha kuku (Fowl Cholera).
• Homa ya matumbo
• Ini.

6**. Konfrei:**



• Ina madini na vitamini nyingi.
• Hutibu vidonda na majipu.

7**. Ndulele (Dungurusi, Makonde, Tura/Ndula):**



• Majani hutibu Minyoo. • Matunda hutibu Vidonda.

8. **Papai (Majani):**



Chemsha magao mawili ndani ya maji lita 6 hadi ubakie na lita 1. Poza kisha chuja. Hutibu: Minyoo
**Pia Majani Ya Mpapai Ni** Dawa ya kutibu Kuku Kuharisha namna yoyote
**Kuandaa** Pata jani moja bichi la Mpapai na uliponde ponde lilainike kiasi. Kisha changanya na maji kiasi cha lita mbili na nusu. Kutumia (kwa tiba) - Kuku wapewe maji hayo wanywe,wasipewe maji mengine kwa ajili ya kunywa kwa siku angalau nne au zaidi.
- Inafaa zaidi kila siku kuwaandalia dawa mpya ili dawa isiharibike.
**Kutumia (kama kinga)** - Hata kama kuku hawaharishi, wakizoeshwa kunywa maji yenye majani ya mpapai yaliyopondwa angalau mara tatu kwa wiki watakingwa magonjwa mengi. Njia nyingine ya kutumia Mpapai: Kuandaa na Kutumia - Chukua majani ya Mpapai uyatwange upate kisamvu chake kiasi cha lita 1. - Changanya kisamvu hicho na pumba lita 2. - Waweza kuongezea maji kidogo na kuwapatia kuku wanaoumwa watumie chakula hicho hadi wapone.

Kama kuku ni wachache, andaa chakula wanachoweza kumaliza kwa siku moja ili kisibakie na kuharibika kabla hawajakimaliza.

9**. Mwembe:** Majani magao mawili, ponda na chemsha ndani ya lita 6 za maji hadi ibaki lita 1. Wape kwa siku moja. Mwembe hutibu: • Homa ya matumbo. • Mafua. • Kinga ya Kideri/Mdondo.

10**. Mpera**: Chemsha majani au mizizi. Mpera hutibu: • Tumbo • Vidonda na majipu 11. Minyaa (Cactus): Hii ni aina yenye majani manene-hadi kufikia nusu nchi na mapana hadi kufikia upana wa viganja viwili vya mikono.

11.**Minyaa** hutibu: (Angalia inaunguza au kubabua). • Vidonda. • Ngozi. • Uzazi

12**. Pilipili Kichaa**:



Pondaponda kiasi kisha changanya na maji na wawekee kuku wawe wanakunywa kwa muda wao.
Inasemekana inasaidia kutibu Mdonde (lakini mapema kabla maradhi kuingia).
Chukua pilipili 5 za kichaa au ndefu au mbuzi kama ukikosa zote, twanga weka kwenye maji lita 4,wape baada ya kula. Wape kwa siku 5 _Hutibu aina zote za mafua.

**13.Kitunguu swaumu:**



Hutibu Mafua,Typhoid,Kuharisha kinyesi cheupe
Jinsi ya kutumia Unakitwanga kisha uchanganya kwenye maji chuja kwa chujio ili kuondoa nyuzi na uchafu. Kiwango cha kuwapa kitategemeana na idadi ya kuku.
Huu ni ushuhuda wa mfugaji alie wahi kutumia kitunguu swaumu kwa kuku wake "[*"Mimi nilitumia vitunguu vinne nikatwanga kisha nikachanganya na maji glasi moja na nusu zile za plastic kisha nikachuja nikawa nawapa na kijiko Mara mbili kwa Siku nilikuwa namshika mmojammoja nampa ili kuhakikisha wanapata dawa*

*wote nikimaliza nawawekea maji ya vitamin wasipoteze hamu ya kula ukiwapa vizuri Siku mbili tu unaona wanapata nafuu"*]

**Tumia Dawa Za Asili Kabla Ya Ugonjwa Haujakiomaa**


***Kumbuka chanjo kwa kuku ni muhimu***

## MFANO WA KUTENGENEZA CHAKULA CHA KUKU KWA MFUGAJI

| Vichanganyio | Kuku Wadogo | Kuku Wakubwa |
|---|---|---|
| Pumba za mahindi | 40Kg | 50Kg |
| Mahindi ya kuparaza | 10Kg | 10Kg |
| Mashudu (Pamba / Alizeti | 20Kg | 10Kg |
| Dagaa / Soya | 24Kg | 15Kg |
| Unga wa mifupa (Bone meal) | 5.25Kg | 5Kg |
| Chokaa ya kifusi | - | 9.25Kg |
| Chumvi | 0.5Kg | 0.5Kg |
| Premix ya broiler | 0.25Kg | - |
| Premix ya layers | - | 0.25Kg |
| **TOTAL** | **100Kg** | **100Kg** |

## PLAN ZA MABANDA YA KUKU




Wire Mesh
with Curtains
Iron Sheets
Ridge with
Curtain
12'
8'
20 ft
50ft
Wall two
blocks High